SIGNAL Publishers
igniting thinking

GREDI YA 9 - 2025

THE SCHOLAR
004

SIGNAL CBC ASSESSMENT
JARIBIO LA NNE

JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

– KISWAHILI KARATASI YA 1–

MUDA: SAA 1 DAK 30

JINA:

.....

GREDI:

.....

SHULE:

.....

NAMBARI YA TATHMINI:

.....

Maagizo kwa mwanafunzi:

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Soma kila swali kwa makini
3. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
4. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.
5. Nakili sahihi yako katika kiapo kilicho chini ya ukurasa huu.

JEDWALI LA ALAMA

Zoezi	Alama za jumla	Alama za mwanafunzi	Upeo
Sehemu A: Ufahamu	25		
Sehemu B: Kihasho	10		
Sehemu C: Sarufi	15		
	50		

Kiapo: "Naapa kutokiuka sheria zozote wakati wa mtihani huu".

Sahihi: ..... **Tarehe: .....**

SEHEMU A: KUSOMA UFAHAMU (alama 25)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 9

Hapo zamani za kale, katika nchi ya Nuru, paliishi kijana aliyeitwa Mwamba. Kijana huyo alienziwa sana na wakazi wengine kutokana na nguvu na jitihada zake za kuitetea jamii yake. Wakazi wengi walitegemea kilimo cha mimea na ufugaji wa wanyama. Mara kwa mara, mahasidi zao waliwavamia kwa **azma** ya kuiba mifugo lakini kila walipofika, Mwamba aliwaongoza mashujaa wenzake wakawasukuma maadui wale hadi nje ya mipaka yao. Wale waliodiriki kuonyesha ukaidi waliangushwa na upanga wa Mwamba.

Miaka ilizidi kusonga hata ukafika wakati wa Mwamba kupata jiko. Alitafutiwa mabinti wote warembo kutoka jamii yake lakini akakataa katakata kuwaoa. Alisema kwamba anataka mke katika nchi ya mbali. Wazee wake walimpa radhi zao akafunga safari asubuhi moja.

Baada ya kupiga milundi kwa juma zima, Mwamba alijipata katika nchi ya Mavuno. Wenyeji wa huko walikuwa waja wakarimu na wenye mioyo safi. Mwamba alipokelewa kwa mikono miwili na kila familia aliyoitembelea. Mabinti wa huko walikuwa hurulaini. Haukupita muda, Mwamba akampata mmoja aliyempendeza akaamua kumwoa.

Utamaduni wa Mavuno ulimhitaji mtu amsaidie baba mkwe katika kazi zake kwa mwezi mmoja kabla ya kukabidhiwa mke. Baada ya hapo, mtu na mchumba wake wangepelekwa mbele ya baraza la wazee wafanyiwe tambiko ili kuwakinga dhidi ya mikosi ya aina yoyote. Mwamba alipoarifiwa hayo, alicheka hadi mbavu zikavunjika. Alidai kwamba yeye alikuwa radhi kulipa kiasi chochote cha mahari almradi asishiriki utamaduni wowote wa kishenzi. Juhudi za kumrai asipuuze kaida hizo ziliambulia patupu. Mwishowe wazee wakaamua kuwa, mtoto akililia wembe mpe.

Mwamba alimchukua mchumba wake bila baraza za wazee akashika tariki kurudi nyumbani. Moyoni aliona fahari kwa ushindi wake. Njiani alikuwa akiimba nyimbo ambazo kwa kawaida waliimba na wenzake kila walipopata ushindi dhidi ya mahasimu.

Signal Publishers Limited 2025
Website: www. signalpublishersltd.com. Email. info@signalpublishers.com
Signal Publishers @Signal Publishers

CamScanner